

MAELEZO YA NAMNA YA KUJAZA FOMU ZA WANACHAMA WA NHIF

A. SEHEMU YA 1: PICHA ZA WANACHAMA

a) Namba ya utambulisho. Mtumishi atajaza namba ya cheki na faili (FN) yake au ya kitambulisho cha kazi. (FN).

b) Picha: Hapa panatakiwa kubandikwa picha za watakapo tengenezewa vitambulisho. Visanduku vimewekwa namba ambazo zitawiana na taarifa za wahusika zilizo sehemu ya 2 na ya 3 katika fomu hii. Zingatia kuwa kisanduku namba 1 ni picha ya mtumishi mchangiaji na namba 2 ni picha ya mwenza (mke/mume).

Yeyote katika wategemezi wanne (watoto wa kuwazaa/kuasili, wazazi au wakwe) anaweza kuwekwa picha yake kuanzia kisanduku namba 3 hadi 6, ila ni muhimbu kuoanisha namba ya kisanduku na taarifa za mwenye picha ili kuepuka kuchanganya picha na majina.

Zingatia kuwa picha zinatakiwa kuwa na ukubwa wa 4.5cm kwa 3.5 na kuwa na rangi ya bluu (clear blue background)

B. SEHEMU YA 2: (TAARIFA ZA MWANACHAMA MCHANGIAJI)

Mtumishi ajaze kikamilifu taarifa zake mara zote anapojaza fomu hii ili kuweza kumtambua kwa urahisi

C. SEHEMU YA 3: TAARIFA ZA WATEGEMEZI

Taarifa za wategemezi zijazwe kikamilifu. Namba 02 ni taarifa za mwenza ambaye picha yake imebandikwa kisanduku namba 02. Kama mwenza hayupo kisanduku na sehemu 02 huachwa wazi.

Sehemu 03 hadi 06 hujazwa taarifa za wategemezi kwa kuzingatia picha zilivyobandikwa.

D. SEHEMU YA 4: UTHIBITISHO WA TAARIFA ZA MWANACHAMA

Mwanachama atapaswa kujaza jina lake na kusaini pamoja na tarehe aliyojaza taarifa zake.

E. SEHEMU YA 5: UTHIBITISHO WA MWAJIRI

Fomu ikishajazwa na mwanachama, mwajiri au mwakilishi wa mwajiri wake atathibitisha ujazwaji kuwa umefanyika kikamilifu na viambatanisho vyote vipo. Ataandika majina yake, cheo chake tarehe aliyothibitisha pamoja na kugonga muhuri wa ofisi.

Fomu zilizojazwa zipelekwe ofisi ya NHIF mkoa iliyo karibu kwa ajili ya utengenezwaji wa vitambulisho

MAELEKEZO MUHUMIMU KWA WANACHAMA

Ili kupata kadi za uanachama wa Mfuko mwanachama anapaswa kujaza fomu hii ya uanachama. Mwanachama ana fursa ya kuweka mwenza wake halali wa ndoa na wategemezi wanne. Hata hivyo siyo lazima mwanachama kujaza nafasi zote kama bado hajapata viambatanisho husika. Anaweza kujaza kwanza kwa ajili yake na baadaye atajaza tena fomu nyingine kuwaweka wale ambao bado hakuwaombea vitambulisho awali.

Ili kupata vitambulisho viambatanisho vifuatavyo vitahitajika

- 1. Mchangiaji:** Hahitaji kiambatanisho chochote tofauti na picha yake
- 2. Mwenza (mke/mume):** Picha yake na nakala ya cheti cha ndoa kikionesha majina yao kikamilifu
- 3. Watoto, wa kuwazaa (biological children):** Picha zao na cheti cha kuzaliwa, na pale mtoto anapokuwa zaidi ya miaka 18 itampasa mwanachama kuambatanisha nakala ya kitambulisho hai cha shule/chuo kuonesha kuwa anasoma
- 4. Watoto wa kuasili (adopted children):** Kibali cha kuasili (adoption order) kutoka mahakama ya hakimu mkazi au Mahakama kuu. (affidavit hazipokelewi)
- 5. Wazazi wa mchangiaji:** Picha zao na nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mchangiaji kikionesha majina ya wazazi wake kikamilifu
- 6. Wazazi wa mwenza(wakwe):** Picha zao na nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mwenza kikionesha majina ya wazazi wake kikamilifu